Toleo 19

# Ukweli wa Injili

MAFUNDISHO YA BIBLIA NA HIMIZO KWA KAZI YA KIMISHENI ULIMWENGUNI KOTE

## SENTI YA MJANE

*(Nakala hii ni ya hadithi ya Yesu kama alivyoitoa katika Marko 12:41-44).*

Yesu aliingia pale uwanjani mwa hekalu na kukaa chini huku akiwatazama watu. Kwa kweli kulikuwa na mchanganyiko wa halaiki ya watu. Kulikuwa na wengine ambao walikuwa wakifanya biashara huku wakinunua na kuuza na kuwachezea shere wale ambao hawakuwa budi kununua wanyama hapo. Kulikuwa pia na Wayahudi kutoka mbali ambao walikuwa wamejaa vumbi na uchovu kutokana na safari ndefu huku wakijiandaa kuleta dhabihu zao kwa makuhani. Nao Mafarisayo wakatembea kwa maringo katikati mwa kusanyiko hilo la watu, huku wakifanya maombi kwa sauti kubwa na kujisifu kibinafsi. Lakini wengine walikuwa na unyenyekevu wa kuwa nyumbani mwa Mungu na walionekana kung'aa nyusoni mwao kwa ibada zao walipokuwa wakifanya maombi na kutoa dhabihu zao kwa Bwana Mungu.

Yesu akatazama shughuli zilizokuwa humo na kupata msukumo rohoni mwake alipoona zaidi ya matendo ya watu hao na kutafakari kuhusu kila moyo wa mtu aliyekuwa hapo. Alitambua vizuri kila roho na msukumo wa moyo wa yeyote aliyekuwa humo. Alijua unyenyekevu wa wale waliokuwa nao, na kiburi cha wale waliokuwa na kiburi. Akaona "utakatifu" wa kibinafsi na tamaaa ya wengine ilhali kwa wengine aliona roho zilizonyenyekea na zilizojaa toba na moyo wa kujinyima.

Tarumbeta ikalia. Yesu na watu wengi wengine waliokuwa kwenye umati



wakageuka na kumwona Mfarisayo akiweka sadaka kubwa kwenye hazina ya hekalu. Hapo kulikuwa na masunduku kadhaa ya kupokea sadaka kutoka kwa watu. Yesu akatazama kwa makini jinsi watu walivyokuwa wakitembea hadi kwenye masanduku hayo na kuangusha pesa zao kwenye hazina ya hekalu. Wengine waliangusha pesa zao kwa unyamavu mkubwa huku wengine wakizipeperusha juu ili kila mtu aone sadaka kubwa waliokuwa wakitoa. Akaona familia moja changa wakiangusha sadaka yao humo kwa haraka kama kwamba wanaona aibu kutokana na kiasi kidogo walichokuwa wakitoa. Pia akaona watu wengi waliokuwa wamevalia vizuri wakitoa pesa nyingi.

Huku Yesu akiwa angali anatazama yaliyokuwa yakiendelea alimwona mjane mmoja maskini sana akitupa senti mbili kwenye hazina hiyo. Senti hiyo ilikuwa ndio sarafu ndogo kabisa iliyotumiwa na Wayahudi wakati huo, na thamani yake ilikuwa ndogo sana. Uso wa Yesu ukang'aa kwa upendo na huruma alizohisi Kristo. Mwanamke huyu alikuwa ametoa pesa za mwisho ambazo alikuwa nazo kumtolea baba yake Mungu. Sasa hakubakisha chochote cha kununua chakula usiku huo lakini alikuwa ametoa yote kwa roho ya kumwabudu Mungu na kumtolea dhabihu.

Yesu akasimama na kuwaita wanafunzi wake kuja kwake. Walipokusanyika karibu naye akaanza kuwanenea. Kundi hilo ambao lilikuwa limemzunguka Yesu likaanza kuwa kubwa wakati watu walianza kuvutiwa na mambo ambayo

*(Inaendelea kutoka ukurasa 2)*


| Tahariri | Kujifunza Biblia:Mafundisho ya Biblia Kuhusu Funfu la Kumi na Kutoa | Mafundisho ya Biblia Kuhusu Funfu la Kumi na Kutoa | Maswali na Majibu | Je, Wajua? Neno Linalofaa kwa Msimu Huu |
|---|---|---|---|---|
| 3 | 4 | 5 | 7 | 8 |

# Mambo Ambayo BIBLIA Inafundisha Kuhusu...

**Neno la Mungu**
2 Tim. 3:6, 2 Pet. 1:20-21, Mt. 24:35
**Uhusiano wa Upendo**
Mt. 22:37-40, Yn. 14:21-23, 1 Yoh. 4:7-21
**Toba**
Mdo. 3:19, 17:30, 2 Kor. 7:10
**Uzao Mpya**
Yn. 3:3-7, 2 Kor. 5:17, Rum. 6:1-4, Efe. 2:1, 5-6
**Uhuru Kutokana na Dhambi**
1 Yoh. 5:18, Mt. 1:21, Yn. 8:11
**Ujazo wa Roho Mtakatifu**
Mdo. 19:2, 15:8-9, 1:8
**Utakatifu**
Lk. 1:73-75, Ebr. 12:14, 1 Pet. 1:15-16, Tit. 2:11-12, Rum. 6:22
**Ufalme wa Mungu**
Lk. 17:20-21, Rum. 14:17, Yn. 18:36
**Kanisa**
Mdo. 2:47, Efe. 4:4-6, 1 Kor. 12:12-13, Kol. 1:18
**Umoja**
Yn. 17:20-23, Gal. 3:28, Ufu. 18:2-4
**Kanuni za Kanisa**
Mt. 28:19-20, 26:26-30, I Kor. 11:23-27, Yn. 13:14-17
**Uponyaji wa Kiungu**
Lk. 4:18, Isa. 53:4-5, Yak. 5:13-16
**Utakatifu wa Ndoa**
Mt. 19:5-6, Lk. 16:18, Rum. 7:2-3, I Kor. 7:10-11
**Urembo wa Nje**
I Tim. 2:9-10, I Kor. 11:14-15, Kum. 22:5
**Mwisho wa Nyakati**
2 Pet. 3:7-12, Yn 5:28-29, 2 Kor. 5:10, Mt. 25:31-46
**Kupenda Amani**
Lk. 6:27-29, 18:20
**Ibada**
Yn. 4:23-24, Efe. 5:19, 2 Kor. 3:17
**Wajibu Mkuu**
Mk. 16:15

*(Endelea kutoka ukurasa 1)*

walikuwa wakisikia: "Huyu mjane maskini ametoa zaidi kuliko wengine wote wanaotia pesa katika sanduku la hazina." Huku watu hawa wakimtazama Yesu kwa mshangao mkubwa, Yeye aliendelea kuwaelezea, "Hao wote wametoa kutokana na wingi wa mali yao, lakini huyu mwanamke katika umaskini wake ametoa vyote alivyokuwa navyo, hiyo ndio riziki yake yote."

Hadithi hii rahisi ya Kristo kuhusiana na senti ya mjane imejaa mafundisho makubwa na inadhihirisha mtazamo wa Mungu kuhusiana na swala la kupeana na kutoa sadaka katika siku zetu. Mungu angali anatazama na kuona wingi wa mali ya matajiri na ufukara wa maskini. Yeye huona yanayotendeka hadharani na kwa siri. Anajua roho inayosukuma watu kutoa sadaka, iwe kwamba inatolewa ili kuonekana na wanadamu ili kupata sifa na heshima ama imetolewa kutokana na upendo wa mtu na kujitolea kwake kwa Mungu.

Mungu huwa na thamani kubwa kuhusu roho inayomsukuma mtu kutoa hata kuliko thamani ya sadaka yenyewe. Yeye anaheshimu sana moyo ambao umejitolea kwake na ambao hutoa kwake hata katika umaskini mkubwa. Hata ingawa sadaka kubwa huwa ni msaada mkubwa kwa kazi ya Mungu mtu haweki hazina Mbinguni kulingana na kiasi cha pesa anachotoa wala sio kulingana na asilimia anayotoa bali ni kulingana na kiwango cha kujinyima. Matajiri wengi huendelea kutoa kulingana na wingi wao wa mali, na maskini wengi nao hukosa kutoa hata kidogo kutokana na umaskini wao. Yesu anafanya mwito kwetu ili sote tuwe na roho na moyo wa mjane aliyekuwa maskini. Tunahitaji kutoa kwa kujinyima iwapo tu matajiri au maskini. Toa sadaka zako sio kutokana na wingi wa mali yako bali kutokana na kiwango chako cha kujinyima.

—mws

## UKWELI WA INJILI

Gazeti la '*Ukweli wa Injili*' huchapishwa kwa jina la Bwana kwa matumizi ya watu wa mataifa yote kwa kusudi la kuimarisha na kuwahimiza watu wote katika ukweli wa neno la Mungu. Gazeti hili hufundisha na kueneza ukweli wa Biblia ambao umethibitishwa tangu nyakati za Yesu Kristo na mitume.

Neno la Mungu ndio mwongozo halisi na wa kipekee wa imani. Linafundisha wokovu na ukombozi kutokana na dhambi unaoletwa na utakaso wa Yesu Kristo; ambao hufuatiwa na ujazo wa Roho Mtakatifu anayemwongoza mhudumu, kumwonyesha njia, na kumpatia nguvu; pia unamletea mtu utakatifu halisi katika kila fani ya maisha yake; na pia kuleta umoja na utangamano wa watu wa Mungu. Huduma inayokubalika na Mungu inatokana na mtu kuwa na uhusiano wa kibinafsi na wa upendo ambao msingi wake ni ukweli.

Waandishi: Michael na René Smith

## UAGIZAJI

*Ukweli wa Injili* ni gazeti la kieletroniki linalochapishwa kila robo ya mwaka kwa jinsi Mungu anavyotuongoza. Tutembelee katika tovuti yetu ya www.thegospeltruth.org ili uagize jalida hili kupitia kwa orodha yetu ya anwani pepe na upokee toleo lako la wakati huu. Hebu jisikie huru kututumia orodha ya majina na anwani pepe za watu wengine ambao wangependa kupokea toleo hili kutoka kwa mwandishi wa jalida la Ukweli wa Injili.

## WASILIANA NASI

Gazeti a Ukweli wa injili linachapishwa katika mataifa mbalimbali ili kusambazwa katika maeneo hayo. Kazi hii na zingine za kimishenari ambazo sisi hufanya huwezekana kupitia kwa matoleo ya kujitolea yanayotolewa kwa jina la Kanisa la Mungu.

The Gospel Truth, P.O. Box 2042, Nixa, MO 65714 USA
editor@thegospeltruth.org

# Tahariri



*Je! Mwanadamu atamwibia Mungu?* – Malaki 3:8

Nabii Malaki aliuliza watu wa Israeli kama walikuwa wamemwibia Mungu, halafu akawaambia kwamba kwa kweli walikuwa wamemwibia Mungu kwa zaka (fungu la kumi) na sadaka. Lakini andiko hili hutumiwa vibaya na visivyo na wahubiri wengi wa uongo ambao hujaribu kushurutisha watu kutoa pesa. Katika baadhi ya nchi ambazo mimi nishazuru hili ndilo huwa somo kuu la huduma katikati ya makusanyiko—fungu la kumi, fungu la kumi, fungu la kumi.

Mzigo ambao niko nao katika robo hii ya mwaka ni kujengea juu ya msingi wa jalida la 18 ambalo nilifundisha kuhusu agano mbili. Fungu la kumi ni mafundisho ya Agano la Kale ambayo yamebatilishwa kwa agano bora zaidi ambalo mtu hutoa kwa uhuru na kutokana na moyo wake wa kibinafsi. Mimi ningependa kwamba watu wangetambua na kupata ujuzi wa baraka za kweli na thawabu ya mtu kujitoa mwenyewe kuhudumu na kutoa. Somo hili la kutoa linaweza kuwa ngumu kwa mtumishi wa Mungu kufundisha kwa sababu watu wanaweza kufikiri kwamba anafundisha ili kujinufaisha kibinafsi. Lakini ni somo muhimu sana na linahitaji kati ya Wakristo wa sasa.

Jukumu la kutoa fungu la kumi haliko lakini wajibu wa kutoa ungaliko. Watu wengine hutoa kiasi kidogo sana kwa sababu hawajafungwa na fungu la kumi la sheria; lakini hebu tukumbuke wito wa Paulo: "Maana ninyi, ndugu, mliitwa mpate uhuru; lakini uhuru wenu usiwe sababu ya kuufuata mwili" (Wagalatia 5:13).

Kuna mahitaji mengi kazini mwa Mungu na sina nafasi ya kutaja mahitaji hayo moja kwa moja. Lakini nitataja mawazo makuu ya kuzingatia kuhusiana na swala la mtu kutoa kwa huduma. Wajibu wa kwanza ni kumtolea yule ambaye anatulisha chakula cha kiroho kila Jumapili—maanake mchungaji wako. Kunaweza kuwa na wakati ambapo mchungaji hayuko ameenda safari. Ni muhimu kwa kusanyiko lake lisisahau wajibu wake wakati kama huo.

Mishenari na Wainjilisti hawana kikundi chochote kimoja cha watu ambacho huchukua jukumu la kuwaunga mkono. Kusafiri safari za nyumbani na za nchi za mbali huwa na gharama kubwa na watumishi hawa wanahitaji kulipa gharama za maisha kama wale wengine. Kutoa sadaka ya wakati moja ni jambo nzuri lakini bora zaidi ni kuwaunga mkono kwa utaratibu na kwa kufuata ratiba fulani. Wakati mhudumu wa injili anapewa sadaka kubwa fahamu kwamba huenda mhudumu huyo amefanya kazi kwa miezi kadhaa huku akipokea msaada kidogo sana, kwa hivyo Mungu anatumia nafasi hiyo kumsaidia.

Kutoa ni jambo lililo na baraka kubwa na sio matajiri tu wanaowajibika kutoa. Iwapo tuna kidogo au nyingi inahitaji kuwa jukumu letu la furaha na shauku kumtolea Bwana sadaka. Mimi nimetambua ukweli kwamba hata tunapojihisi kwamba hatuna uwezo wa kutoa, wakati tunapomtii Bwana, Yeye hukutana na mahitaji yetu. Kwa kweli hatuwezi kutoa zaidi ya jinsi Bwana Mungu anavyotupatia.

Michael W. Smith

Januari 2017

*mengi kwa*
MTANDAO

*Tutembelee kwa*

*www.thegospeltruth.org*

*ili uagize na kusoma*

*jarida letu.*

**Kusimamia Fedha Za Kanisa**

Wanafunzi wa Yesu walikuwa wameshughulika sana ili kuhudumu Neno la Mungu na wakawashauri watu: "chagueni watu saba miongoni mwenu, walioshuhudiwa kuwa wema, wenye kujawa na Roho, na hekima, ili tuwaweke juu ya jambo hili" (Matendo 6:2-3). Mashemasi ndio walio na wajibu katika biblia kusimamia shughuli za kanisa. Kuaminika na uwazi ni jambo muhimu katika mambo ya kifedha.

Kwa kawaida si jambo nzuri kwa mhudumu wa Injili kuwa ndiye anashughulikia pesa za kanisa. Na pia ni jambo la busara ikiwa mhudumu huyo hatajua ni nani katika kusanyiko lake anayetoa na kwamba anatoa kiasi gani ili asiathiriwe visivyo na habari hiyo.

# MWONGOZO WA KUJIFUNZA BIBLIA

## SOMO: MAFUNDISHO YA BIBLIA KUHUSU FUNGU LA KUMI NA KUTOA



### TENDO NA THAWABU YA KUWA MTU MTIIFU

Yesu alisema, “Wapeni watu vitu, nanyi mtapewa; kipimo cha kujaa na kushindiliwa, na kusukwa-sukwa hata kumwagika” (Luka 6:38). Kuna baraka kubwa ambayo watu wengi hukosa wakati wanakosa kumpatia Bwana mazao yao ya kwanza kwa njia ya kujinyima. Maisha ya Wakristo yanahitaji kudhihirika kupitia kwa mioyo yao ya ukarimu.

Kuna vikundi kadhaa vya watu ambavyo vinahitaji msaada wako wa kifedha—tu (wengi) ambao wana mahitaji, juhudi za kueneza injili, na wafanyi kazi shambani mwa Bwana. Mtume Paulo alimwambia Timotheo kwamba, wale watendao mema wawe matajiri kwa kutenda mema, na wawe tayari kutoa mali zao na ndipo watajiwekea akiba iwe msingi mzuri kwa wakati ujao, na ili wapate uzima ulio wa kweli (1 Timotheo 6:18-20).

**Somo la Biblia:** *Katika mambo yote nimewaonyesha ya kuwa kwa kushika kazi hivi imewapasa kuwasaidia wanyonge, na kuyakumbuka maneno ya Bwana Yesu, jinsi alivyosema mwenyewe, Ni heri kutoa kuliko kupokea.* —Matendo 20:35

**Muhstasari:** Fungu la kumi lilikuwa wajibu ambalo liliamuriwa kufanywa katika Agano la Kale. Lakini agano jipya likatanguliza mfumo wa kutoa ambao ulikuwa wa uhuru, wa kujinyima, na wa kutoka katika moyoni wa mtu. Utoaji katika Agano Jipya hauongozwi na asilimia ya mapato bali ni kwa kulingana na upendo na kujinyima kwa roho ya mtu.

**I. Utoaji wa Fungu la Kumi Kabla ya Sheria Kuingia**
- A. Mwanzo 14:17-20 Ibrahimu atoa fungu la kumi kwa Melkizedeki.
- B. Mwanzo 28:20-22 Yakobo amwahidi Mungu kwamba atamtolea fungu la kumi.

**II. Kutoa Fungu la Kumi Katika Sheria ya Musa**
- A. Walawi 27:30-33 Mungu anaamuru kutolewa kwa fungu la kumi la kikulima.
- B. Hesabu 18:21-24 Fungu la kumi la Walawi.
- C. Kumbukumbu 14:22-23 (12:6-7) Amri ya kutolewa kwa fungu la pili la kumi.
- D. Kumbukumbu 14:28-29 (26:12-13) Fungu la kumi la maskini linaanzishwa.
- E. Malaki 3:8-9 Israeli wamwibia Mungu.

**III. Sheria ya Musa si ya Wakati Huu**
*(tazama toleo la 18)*
- A. Waebrania 8:6-13 Agano Jipya linaanzishwa.
- B. Mathayo 23:23 Yesu awakemea viongozi waliokuwa wakitoa fungu la kumi.
- C. Warumi 7:6 Kukombolewa kutokana na Sheria.

**IV. Kupeana katika Agano Jipya**
- A. II Wakorintho 9:6-7 Sadaka za kutolewa kwa moyo mkunjufu na kwa kujitolea zinaanzishwa.
- B. Yakobo 2:14-18 Ishara ya imani ya kweli.
- C. Waefeso 4:28 Fanya kazi ili uweze kupeana.

**V. Njia Inayofaa ya Kupeana**
- A. Mathayo 6:1-4 Bila kujulikana.
- B. II Wakorintho 8:1-5 Kwa kujinyima na kwa kujiamulia mwenyewe (Marko 12:41-44).

**VI. Kiwango cha Kupeana**
- A. II Wakorintho 9:7 Kama ulivyojiamulia moyoni.
- B. I Wakorintho 16:1-2 Kama Mungu alivyokubariki.
- C. Matendo 11:29 Kulingana na uwezo wako.
- D. Matendo 5:1-11 Uamuzi wa kibinafsi (mstari wa 4).

**VII. Kuwasaidia Wahitaji**
- A. I Timotheo 5:16 Wajane.
- B. Yakobo 1:27 Mayatima.
- C. Warumi 15:25-26 Wakristo maskini (Matendo 11:27-29).
- D. Wagalatia 6:9-10 Wa nyumba ya imani.
- E. Yakobo 2:14-18 Wasio na mavazi na wenye njaa.

**VIII. Kuisaidia Huduma**
- A. I Wakorintho 9:7-14 Usimfunge kinywa ng’ombe apurapo nafaka.
- B. Wagalatia 6:6 Kuwasaidia waalimu.

**IX. Baraka ya Kupeana**
- A. Matendo 20:35 Ni baraka zaidi kutoa.
- B. Luka 6:38 Wapeni watu vitu, nanyi mtapewa.
- C. Wafilipi 4:18 Inampendeza Mungu.
- D. I Timotheo 6:18-19 Uzima wa milele.

**Tamati:** *Mmepata bure, toeni bure.*
—Mathayo 10:8b

# MAFUNDISHO YA BIBLIA KUHUSU FUNGU LA KUMI NA KUTOA

### Historia ya Fungu la Kumi

Fungu la kumi ni mafundisho ya Agano la Kale ambayo yamebadilishwa katika Agano Jipya ambapo mtu hutoa sadaka kwa Bwana kwa njia ya kujichagulia, maanake kwa hiari yake mwenyewe. Ni jambo muhimu mtu kujua na kuelewa historia na mafundisho ya Biblia kuhusiana na swala hili. Mara mbili kabla ya nyakati za sheria ya Musa tunakutana na watu ambao walitoa zaka (fungu la kumi). Katika Mwanzo 14:17-20 Ibrahimu alimtolea Melkizedeki (ambaye alikuwa mfalme na kuhani wa Salemu) fungu la kumi. Zaka hiyo haikutokana na mapato ama wingi wa mimea bali ilitokana na faida ambayo alipata kutokana na ushindi vitani. Katika Mwanzo 28:20-22 Yakobo alifanya nadhiri mbele zake Mungu na kumwahidi kwamba angempa fungu la kumi kama Mungu angekutana na mahitaji yake. Lakini katika nyakati zote mbili Mungu hakutoa amri ya kutolewa fungu la kumi, ilikuwa tu watu hawa kutoa kwa kupenda na kwa hiari na kwa kujitolea kwao wenyewe.




### Sheria ya Musa

Katika Sheria ya Musa watu waliamuriwa kutoa fungu la kumi. Lakini fungu la kumi linalopatikana katika Agano la Kale ni tofauti na ile ambayo inafundishwa na makanisa ya kisasa. Kulingana na Walawi 27:30-32 fungu la kumi lilitokana na ukulima na lilitolewa kutoka kwa mifugo na mimea, na sio kutokana na mshahara.

### Zaka Tofauti Tofauti Zinazoamuriwa Katika Agano La Kale

Zaidi ya hayo, hata ingawa zaka ilijumuisha asilimia kumi ya mapato, kulikuwa na zaka tofauti tofauti ambazo zilihitajika kutolewa kulingana na sheria ya Agano la Kale. Kwa hivyo, kiwango kile mtu alitakiwa kutoa kilikuwa zaidi ya asilimia kumi ambayo leo inapigiwa debe. Ingawa kuna maoni tofauti tofauti kuhusu asilimia ambayo iliamuriwa katika sheria ya Musa, kulikuwa na asilimia ishiriri zingine ambazo zilihitaji kutolewa katikati mwa zaka za fungu la kumi.

### Zaka ya Walawi

Walawi hawakupewa urithi katika nchi ya Israeli pamoja na makabila yale mengine kwa sababu walitumika kwa mambo ya kidini kwa ajili ya wana wa Israeli. Zaka ya mwaka wa kwanza, maanake zaka ya Walawi, iliamuriwa kutolewa kwa ajili ya kuwasaidia Walawi na makuhani wa wana wa Israeli ili waweze kukutana na mahitaji yao: "Na wana wa Lawi, nimewapa zaka yote katika Israeli kuwa urithi wao, badala ya huo utumishi wautumikao" (Hesabu 18:21). Walawi na makuhani walipewa fungu la kumi kama mshahara kwa njia kwa ajili ya utumishi na kujitolea kwao.

### Zaka ya Sherehe

Kulikuwa na zaka ya pili ambayo ilikuwa ni ya sherehe, ambayo iliamuriwa kuletwa kwenye hema ya makutano au hekaluni kwa ajili ya sherehe na karamu za kidini katika nchi ya Israeli. "Usiache kutoa zaka ya fungu la kumi katika maongeo yote ya mbegu zako, yatokayo shamba mwaka baada ya mwaka.
Nawe utakula mbele za Bwana, Mungu wako, mahali atakapochagua apakalishe jina lake, zaka ya nafaka zako, na divai yako, na mafuta yako, na wazaliwa wa kwanza wa makundi yako ya ng'ombe na ya kondoo; ili upate kujifunza kumcha Bwana, Mungu wako, daima" (Kumbukumbu 14:22-23). Washirika wa familia na watumishi wa nyumba hiyo ndio walikula zaka hiyo. Huu ulikuwa ni wakati wa furaha na nafasi za wana wa Israeli kufanya zile safari tatu za kwenda mjini Yerusalemu. Basi hii ilikuwa ni zaka iliyokuwa kando ya ile zaka ya kwanza.

### Zaka ya Maskini

Miongozo ilitolewa katika Kumbukumbu 14:28-29 na 26:12-13 kwa zaka ya tatu, zaka ya maskini. Hii zaka haikuwa ya kila mwaka bali ilitolewa katika kila mwaka wa tatu kusaidia wageni, watu wasiojulikana, mayatima, na wajane. Kuna mgogoro kati ya wasomo na hata kati ya waalimu wa Kiyahudi kama kwamba hii zaka ilikuwa tofauti kabisa kutokana na zaka ya pili ama ilichanganywa kwa zaka ya pili na kutolewa kwa maskini katika mwaka wa tatu na wa sita wa kipindi cha sabato. Ni muhimu kuzingatia kwamba zaka ya kwanza ilikuwa inapelekwa katika miji ya Walawi, ya pili ilikuwa ipelekwe Yerusalemu, na ya tatu ilikuwa ya kusaidia maskini "ndani ya malango yako" (Kumbukumbu 26:12). Zaka hii ya maskini iliamuriwa ili maskini wapate msaada "ili kwamba Bwana, Mungu wako,

*(Inaendelea kutoka ukurasa 6)*

(Endelea kutoka ukurasa 5)

akubarikie katika kazi yote ya mkono wako uifanyayo" (Kumbukumbu 14:29).

Kando kando na sadaka yote ya kujitolea ambayo wana wa Israeli wangetoa kiwango cha zaka ya mimea na mifugo kingekuwa zaidi ya asilimia 20%-23.3%. Zaka hizi hazikuwa za mtu kujichagulia mwenyewe bali ziliamuriwa na Bwana Mungu. Basi nabii akauliza wana wa Israeli katika Malaki 3:8-9, "Je! Mwanadamu atamwibia Mungu? Lakini ninyi mnaniibia mimi. Lakini ninyi mwasema, Tumekuibia kwa namna gani? Mmeniibia zaka na dhabihu." Wana wa Israeli walikuwa wakimwibia Mungu kile ambacho kilikuwa chake kwa haki katika sheria ambayo Musa alipeana.



### Agano la Kale Linabadilishwa

Fungu la kumi lililoamuriwa katika Sheria ya Musa lilifanana na ushuru unaotolewa serikalini au katika mambo ya kidini na kusudi lake lilikuwa kukutana na mahitaji ya serikali ya kidini katika nchi ya Israeli, ili kukutana na mahitaji ya kijamii, kidini, na kiserikali. Ni wazi kwamba zaka ilikuwa ni moja ya amri zilizoko kwenye Agano la Kale, lakini kinyume na vile wahubiri wengi wa uongo wanavyofundisha zaka haifundishwi katika Agano Jipya. Wakati Yesu alikuja Yeye alifanya agano jipya na watu wa Mungu na agano la kale likawa halifanyi kazi tena (Waebrania 8:6-13). Mstari wa nane unasema hivi: "Maana, awalaumupo, asema, angalia, siku zinakuja, asema Bwana, nami nitawatimizia nyumba ya Israeli." Mfumo wa sheria ya zaka ulibadilishwa kama ilivyobadilishwa udumishaji wa Sabato, kafara za wanyama, ibada za kimwili, n.k.

Yesu alinena kuhusu utoaji wa fungu la kumi wakati ambapo aliwakemea viongozi wa kidini ambao walikuwa waaminifu kutoa fungu la kumi lakini walikosa kutilia maanani mambo makuu ya sheria (Mathayo 23:23; Luka 11:42). Utoaji wa fungu la kumi lilikuwa jambo ambalo lilikuwa likiendelea wakati wa huduma ya Kristo katikati mwa Wayahudi kwa sababu Israeli ilikuwa ingali chini ya sheria, na mpango kamili wa wokovu haukuwa umekamilika hadi katika siku ya Pentekoste.

Kanuni kadhaa za Agano la Kale zilirudiwa tena, lakini nyingi zake zilikamilishwa kwa kiwango cha hali ya juu cha maisha kwa misingi ya uhusiano wa kibinafsi na wa kujiamulia kati ya mtu na Yesu Kristo. Utakatifu wa kweli haupatikani kwa misingi ya kutoa "zaka katika mapato yangu yote" bali katika neema ya Yesu Kristo yenye kumwokoa mtu. "Bali sasa tumefunguliwa katika torati, tumeifia hali ile iliyotupinga, ili sisi tupate kutumika katika hali mpya ya roho, si katika hali ya zamani, ya andiko" (Warumi 7:6).

### Kupeana Katika Agano Jipya

Hata ingawa Agano Jipya halifundishi utoaji ambao unafanana na "ulipaji wa ushuru" Agano lenyewe lina mengi linalosema kuhusu kupeana. Msingi wa Ukristo ni mtu kujitolea kwa hiari yake mwenyewe na kufanya utumishi wa upendo kwake Mungu. Mafundisho kuhusu utoaji katika agano jipya umefanyiwa muhstasari wake na mtume Paulo anapotoa miongozo kwa kusanyiko la huko Korintho: "Lakini nasema neno hili, Apandaye haba atavuna haba; apandaye kwa ukarimu atavuna kwa ukarimu. Kila mtu na atende kama alivyokusudia moyoni mwake, si kwa huzuni, wala si kwa lazima; maana Mungu humpenda yeye atoaye kwa moyo wa ukunjufu." (2 Wakorintho 9:6-7).

**Kila kitu ambacho Mkristo yuko nacho kinahitaji kuwekwa wakfu kwa Bwana.**

### Kutoa Kwa Uhuru Na Kwa Hiari

Badala ya fungu la kumi sadaka zetu zote kwa Bwana zinahitaji kuwa "sadaka za kujitolea." Kulingana na mchanganuzi wa mambo Adam Clarke Wayahudi walikuwa na masanduku mawili ya sadaka humo kwenye hekalu. Kulikuwa na saduku "la lazima" ambapo sadaka ziliwekwa ambazo zililingana na sheria--maanake fungu la kumi. Sanduku la pili lilikuwa la sadaka za kujichagulia ambako watu hawakutoa kulingana na fungu la kumi lakini kulingana na jinsi walivyompenda Mungu moyoni. Basi katika Agano Jipya sanduku hilo la fungu la kumi limeondolewa na sasa sadaka zinahitaji kutolewa kwa jinsi mtu ameamua moyoni—sio kulingana na amri ya asilimia kumi au ishirini.

### Wajibu Wa Kupeana

Uhuru kutokana na sheria ya zaka hauwaweki watu huru kutopeana mapato yao. Kila kitu ambacho Mkristo yuko nacho anahitaji kukiweka wakfu kwa Bwana. Hata ingawa hakuna asilimiana ambayo Mkristo anatakiwa kutoa, yeye ana wajibu wa kupeana kwa ukarimu, kwa kujinyima, na kwa moyo mkunjufu. Mkristo anapofanya maamuzi kuhusiana na mambo yake ya kifedha yeye anahitaji kulipatia tendo la kumtolea Bwana kipa umbele. Sadaka za maamuzi ya kibinafsi zinahitaji kutolewa ili kuunga mkono huduma ya Bwana, kazi ya injili, maskini, n.k. Tumeombwa "kuyakumbuka maneno ya Bwana Yesu, jinsi alivyosema mwenyewe, Ni heri kutoa kuliko kupokea" (Matendo 20:35). Sadaka za kutoka moyoni mwa mtu ni dhabihu ambazo zinakubalika na kumfurahisha Bwana Mungu (Wafilipi 4:18).

—mws

# MASWALI na MAJIBU

## Njia Muafaka ya wakristo kupeana ni Ipi?

"Wewe utoapo sadaka, hata mkono wako wa kushoto usijue ufanyalo mkono wako wa kuume" (Mathayo 6:1-4). Watoto wa Mungu hawastahili kupeana ili watambuliwe au wasifiwe na wanadamu. Ikiwezekana Wakristo wanahitaji kutoa bila kujulikana, kwa siri, na kwa unyenyekevu mkubwa na upendo.

## Je, Inafaa Kusanyiko la Wakristo Kuchukua Sadaka, Na Kwa Njia Ipi?

Silo tu jambo ambalo linafaa bali pia ni jambo lenye manufaa kwa kusanyiko kutoa nafasi ya watu kumtolea Bwana sadaka. Mtume Paulo alitoa mawaidha kwa kusanyiko la Korintho na kuwaambia: "Kwa habari ya ile changizo kwa ajili ya watakatifu, kama vile nilivyoamuru makanisa ya Galatia, nanyi fanyeni vivyo" (1 Wakorintho 16:1-2). Kanisa hilo lilipewa maagizo ya kuwa na kusanyiko la kifedha katika kila siku ya kwanza ya wiki, ambayo ilikuwa ndio siku ya ibada. Kutoa ni sehemu ya ibada na ni utumishi wa upendo kwa Bwana na ni jambo ambalo halistahili kupuuzwa.

Maandiko hayatoi mwongozo wa moja kwa moja wa jinsi ambavyo sadaka inastahili kuchukuliwa. Lakini sadaka hiyo inahitaji kuwa ya mtu kujiamuria mwenyewe na isiwe ni minyororo ya kufunga watu. Ni jambo muhimu kwamba tusifanye utaratibu mrefu wa kuwawezesha watu kutoa—iwe aidha kwa watu kutoa kupitia kwa sanduku la kumwezesha mtu kutoa kwa siri au ni kwa kutoa hadharani. Lililo muhimu ni kwamba kuweko na uhuru wa watu kutoa na kwamba jambo hilo lifanywe faraghani.Utoaji huu unahitaji kufanywa kwa roho ya unyenyekevu na sio kwa roho ya udalali, roho ambayo baadhi ya makanisa hutumia kukusanya fedha.

## Je, Wakristo Wanahitaji Kutoa Mara Ngapi?

Biblia inafundisha kwamba Mkristo anahitaji kupeana "kama alivyokusudia moyoni mwake" (2 Wakorintho 9:7). Nayo 1 Wakorintho 16:2 inasema, "Kila mtu kwenu na aweke akiba kwake, kwa kadiri ya kufanikiwa kwake." Basi Mkristo anahitaji kutoa kulingana na jinsi Roho anafanya kazi moyoni mwake na kutoa kulingana na kaisi kile




anachojisikia moyoni. Hata ingawa hatuko chini ya sheria ya fungu la kumi, agano la kale lilikuwa ni mwalimu wetu. Basi ni jambo muhimu mtu kumtolea Bwana sadaka kwanza kabla ya mambo mengine yote ya kifedha, kwa kukusudia na kwa desturi. Ni jambo muhimu sana mtu kukusudia kumpa Bwana sadaka na yeye kuwa mwaminifu kwa jambo hilo, na pia kutomwekea Mungu vizuizi wakati Yeye anakuongoza kumpatia zaidi. Kwa watu wale ambao mapato yao ni ya kiwango cha chini kutoa kwa kujinyima kunaweza kuwa ni kutoa kiasi kidogo tu cha fedha. Lakini kwa matajiri kutoa kwa kujinyima kunaweza kuwa ni kutoa zaidi ya asilimia ishirini ya mapato yao. "Na wale wanafunzi, kila mtu kwa kadiri ya alivyofanikiwa, wakaazimu kupeleka msaada kwa ndugu zao waliokaa Uyahudi" (Matendo 11:29).

## Je, Ni Nani Anastahili Kupewa Sadaka?

Silo jambo lazima kutoa kuwe tu kupitia kusanyiko la mahali moja peke yake. Lakini kutoa huko kunahitaji kulingane na miongozo ya Neno la Mungu. Sadaka zinahitaji kutolewa ili kutimiza majukumu ya Kibiblia ya kuwasaidia maskini, wajane (1 Timotheo 5:16), mayatima (Yakobo 1:27), na kuunga mkono huduma na kazi ya Mungu kwa jumla.

Sadaka zilichukuliwa katika kanisa la Makedoni na Akaia kuwasaidia Wakristo maskini waliokuwa Yerusalemu (Warumi 15:25-26). Msaada pia ulitumwa kwa ndugu wa huko Uyahudi (Matendo 11:27 -29). Mtume Yakobo naye alinena kuhusu umuhimu wa imani ya mtu kuonekana kupitia kwa kuwasaidia wasio na mavazi na wenye njaa (Yakobo 12:14-18). Wajibu wa kuwasaidia maskini huanzia katika nyumba ya imani na kusambaa kutoka hapo (Wagalatia 6:9-10). Maandiko pia yako dhahiri yanaposema kwamba tunafanya kazi kwa mikono ili kuwasaidia wahitaji (Waefeso 4:28). Pia tunao wajibu wa kutoa ili kukutana na mahitaji ya kanisa na kutunza mahali pa ibada.

Katika Agano la Kale wana wa Israeli walitakiwa kutoa fungu la kumi ili kuwaunga mkono makuhani na Walawi. Katika Agano Jipya Wakristo wamefundishwa katika mahali kwingi kwamba wanahitaji kuunga mkono huduma kwa njia ya kifedha: "Usimfunge kinywa ng'ombe apurapo nafaka . . . Ikiwa sisi tuliwapandia ninyi vitu vya rohoni, je! Ni neno kubwa tukivuna vitu vyenu vya mwilini?" (1 Wakorintho 9:7-11). Ikiwa wewe unafunzwa Neno la Mungu basi muunge mkono yule ambaye anakufundisha mambo mazuri (Wagalatia 6:6). Mfanyi kazi anastahili mshahara wake, awe ni mchungaji, mwinjilisti, mishenari, n.k. Ni wajibu wa Wakristo kuwaunga mkono (kwa hiari yao wenyewe) wale ambao wanafanya kazi katika ufalme wa Mungu.

JE, WAJUA?

## FIMBO YA FUNGU LA KUMI

"Bwana alianzisha kanuni ya fungu la kumi katika Israeli kwa kutumia mtindo ambao wachungaji walihesabu kondoo wao (Walawi 27:32). Wakati kondoo walikuwa wakiingizwa mahali pao pa kulala mchungaji alisimama hapo huku akiwa na fimbo iliyokuwa na rangi. Mchungaji huyo alimpaka kila kondoo wa kumi aliyeingia malazini rangi kwa kutumia fimbo hiyo. Jambo hilo lilimwezesha mchungaji huyo kuwahesabu kondoo wake kwa haraka ili kutambua kama kuna yeyote wao ambaye alikuwa amepotea."

*(Knight, George W. 2007 Bible Customs & Curiosities [Tamaduni na Mambo yenye Kushangaza katika Biblia], ukurasa wa 56).*

Neno Linalofaa kwa Msimu Huu

## KUISHI KWA INJILI

**Anwani**

The Gospel Truth
P. O. Box 2042
Nixa, MO 65714
USA

Email:
editor@thegospeltruth.org

UTAKATIFU KWA BWANA

*Hamjui ya kuwa wale wazifanyao kazi za hekaluni hula katika vitu vya hekalu, na wale waihudumiao madhabahu huwa na fungu lao katika vitu vya madhabahu? Na Bwana vivyo hivyo ameamuru kwamba wale waihubirio Injili wapate riziki kwa hiyo Injili.*
—1 Wakorintho 9:13-14



Wahudumu hawastahili kuitisha watu fedha kwa ajili ya matumizi yao ya kibinafsi bali wanastahili kuwa na imani kwa Mungu ambaye aliwaita kuhudumu. Wahudumu wa injii hawastahili kufanya kazi ya huduma ili kupata mali iliyoporwa wala kwa sababu ya kupata mshahara, bali wanahitaji kutumika kwa moyo wenye utayari na wenye mzigo wa kujenga Wakristo.

Lakini hata ingawa wahudumu wa Injili wanastahili kumtegemea Bwana na sio wanadamu, kuna wajibu ambao watu wa Mungu wamepewa. Mtume Paulo alikuwa akilikumbusha kanisa la Korintho kuhusu kazi na gharama ya huduma. Katika siku zilizopita makuhani walikuwa na haki ya kupata sehemu ya sadaka ili kujidumisha. Kwa sababu wao walihudumu madhabahuni basi walipata sehemu yao kutoka madhabahuni. Hivyo pia ndivyo inastahili kuwa kati ya watu wa Mungu hata katika siku zetu. Mungu amepanga na amekubali kwamba iwe hivyo; wanaoihubiri injili waishi kutokana na injili.

Wale ambao wametumwa na Kristo kuhuduma na kuweka maisha yao hatarini kwa ajili ya uenezaji wa injili wanastahili kuungwa mkono na kudumishwa kazini mwao. Ni wajibu wa waumini kujinyima na kupeana kwa ukarimu ili huduma hiyo iendelee na kwamba wahudumu waweze kuweka umakini kwa mambo ya Mungu na kuendeleza kazi ya Injili kwa ustadi zaidi humo kwenye shamba la kiroho.

—mws